HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31/05/2018

Mh. Mwenyekiti,

Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango

Hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha kujadili taarifa mbalimbali za Fedha, Uongozi na Mipango. Kikao hiki kinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa agizo namba 21.Kwa msingi huo ni jukumu la kila mjumbe kupitia taarifa hii na kuchangia maoni ambayo yataisaidia Halmashauri kufikia lengo kuu la kutoa Huduma nzuri na endelevu zenye kuleta Maendeleo katika Wilaya yetu ya Mufindi.

1) **Mapitio ya Bajeti 2017/18**

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs.51,837,410,700.05** Makusanyo haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo	Kiasi
1.	Mapato ya ndani	3,890,726,000.00
2.	Ruzuku Mishahara	34,456,072,480.00
3.	Ruzuku matumizi ya kawaida	2,985,977,000.00
4.	Ruzuku ya miradi ya maendeleo na Wadau wengineo	7,172,987,920.05
5	Nguvu za Wananchi	3,331,647,300.00
JUMLA		**51,837,410,700.05**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri imeanza na bakaa ya**Tshs.1,045,869,756.00** Fedha hizi zimegawanyika kama ifuatavyo;

Jina la akaunti	Namba ya akaunti	Kiasi
Matumizi ya kawaida	60210001175	13,576,535.08
Miradi ya Maendeleo	60210001176	590,915,991.91
Maji	60210004850	39,590,304.29

Mapato ya ndani	60210001172	183,421,565.51
Akaunti ya Mishahara	60210001174	114,890,860.00
Elimu	60210018989	195,880.31
Afya	60210018991	103,278,618.90
Jumla		**1,045,869,756.00**

Katika kipindi cha Julai 2017 – Mei 2018 Halmashauri imepokea fedha nje ya makisio ya mwaka kiasi cha **Tshs.2,624,294,254.85**, Kati ya fedha hizo Kiasi cha **Tshs.2,364,791,726.88** ni kwa ajili ya Miradi ya TASAF na **Tshs.118,593,555.04** ni kwa ajili ya Mradi wa Bonde la Kihansi na **Tshs.67,176,132.00** ni kwa ajili ya mradi wa Umeme Vijijini – REA, na **Tshs 36,220,000** ni kutoka UNICEF kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkakati wa Halmashauri Aidha Halmashauri imeongezewa makisio ya nyongeza katika kifungu cha Mitihani ya kidato cha Nne na cha Pili kiasi cha **Tshs.37,512,840.93,**

Mh. Mwenyekiti

Ukijumlisha fedha ya bakaa, makisio yaliyokuwa yameidhinishwa, bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka 2017/2018 na Makisio ya nyongeza inakuwa na jumla ya **Tshs.55,507,574,710.90** kwa mchanganuo ufuatao;

Chanzo cha Mapato	**Kiasi**
Mapato ya ndani	4,047,724,070.59
Ruzuku ya Mishahara	34,570,963,340.00
Matumizi mengineyo	3,052,317,079.77
Nguvu za Wananchi	3,331,647,300.00
Miradi ya Maendeleo	10,504,922,920.54
Jumla	**55,507,574,710.90**

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Halmashauri ya wilaya ya Mufindi inategemea kutumia jumla ya **Tshs.55,507,574,710.90** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	34,589,425,340.00
Matumizi ya Kawaida	5,036,697,826.46
Miradi ya maendeleo	15,881,451,544.44
Jumla	**55,507,574,710.90**

2) Hali Halisi

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha Julai hadi Mei 2018, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya **Tshs.31,439,236,289.40**. Kati ya Mapato haya **Tshs.3,019,593,938.41** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani, **Tshs.22,590,649,480.06** ni Mishahara, **Tshs.3,770,940,934.88 ni** Miradi ya maendeleo na **Tshs.2,058,051,936.05** ni Matumizi ya kawaida. Aidha , katika kipindi cha Julai 2017- Mei 2018 Mchango wa wananchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo ulikuwa na thamani ya Shs **793,525,573.**

Mlinganisho wa Mapato halisi ya **Tshs. 31,439,236,289.40** kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018 na makisio ya **Tshs.54,461,704,954.90** ya mwaka 2017/18 unaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **59.18** ya lengo la mwaka wa fedha wa 2017/18. Aidha mlinganisho wa mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018 ya **Tshs.3,019,593,938.41** na Makisio ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ya **Tshs.3,890,726,000.00** kwa kipindi hicho, yanaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **77.61** ya lengo la mwaka .

Mh Mwenyekiti,

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai 2017- Mei 2018 unaonesha kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato haikuwa ya kuridhisha.

Hali hii inasababishwa na

- Sehemu ya zao la chai inayovunwa kuharibika kabla ya kufikishwa kiwandani kutokana na ubovu wa miundombinu ya usafirishaji na wakati mwingine chai kukatiwa chini kutokana na utaratibu wa uvunaji waliojiwekea wakulima wa chai.
- Wafanya Biashara wa mbao wanaochakata mbao katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kutumia vibali walivyopewa na SAO HILL kusafirisha mbao kuzileta mji wa mafinga hata pale ambapo wamechakata mbao zilizotokana na misitu inayonunuliwa katika mashamba ya watu binafsi.
- Kutokusanya leseni za biashara kama ilivyo kwenye bajeti kutokana na uhaba wa watumishi katika kitengo cha Biashara.
- Kutokamilika kwa mfumo wa upokeaji wa mapato ya mauzo ya viwanja.

Ili kukabiliana na hali hii Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo

- Kufanya doria kila mara ili kuwakamata wanaotorosha mazao ya misitu bila kulipia.Aidha Halmashauri imeunda kikosi kazi kinachohusisha wakuu wa idara na watalaam wengineo kwa ajili ya kufanya Doria
- Kuanzisha/kutenga maeneo ambayo yatatumika kama sehemu ya kuuzia mazao ya misitu kama mbao katika maeneo yanayopatikana mazao haya kwa wingi
- Kila idara kusimamia chanzo cha mapato ili kuhakikisha kinakusanywa kulingana na makisio iliyojiwekea.

- Kusimamia matumizi ya Mfumo wa Ki Electronic wa ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na mashine za Ki electronic za kukusanyia mapato zimeongezwa 20 ili kila Sehemu inayostahili kupata mashine hizi ipatiwe.
- Kuendelea kuwatambua Wafanyabiashara wanaofanya biashara katika Eneo la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Mufindi ili waweze kulipa kodi na Leseni za Biashara.
- Katika Mwaka wa fedha wa 2018/19, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kubadilisha utaratibu wa ukusanyaji wa ushuru wa magogo na mbao kwa kukusanya ushuru wa mbao kwa mbao zote zitakazochakatwa katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na kukusanya ushuru wa Magogo kwa wale wafanya biashara watakaosafirisha Magogo.
- Kuwasiliana na TARURA pamoja na wadau wa chai ili kuona jinsi ya kutengeneza miundombinu iliyopo maeneo yanayolimwa chai.
- Kuanzisha Vituo vya kukagulia Mazao ya Misitu kwa kadiri itakavyoonekana inafaa
- Kuendelea na uhamasishaji kwa Wananchi kuhusu uuzwaji wa viwanja vya Igowole.
- Kuendelea kuhamasisha Jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii
- Kimeundwa kikosi kazi kwa ajili ya kufuatilia leseni za biashara katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri mara mbili kwa wiki kuanzia tarehe 29/5/2018

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti,

Matumizi hutegemea mapato yanayokusanywa. Kwa kipindi cha kuishia 28, Mei 2018, Halmashauri imetumia kiasi cha T**shs.32,328,467,566.89** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo,

Chanzo cha Matumizi	**Kiasi**
Mishahara	22,590,649,480.06
Matumizi mengineyo	4,567,394,316.01
Miradi ya maendeleo	5,170,523,770.82
Jumla	**32,328,467,566.89**

3) Taarifa Nyinginezo

a) Usuluhisho wa Benki

Mh. Mwenyekiti,

Usuluhisho wa benki kwa mwezi Mei 2018 umefanyika kwa akaunti zote nane kama ifuatavyo,

Na	Jina la Akaunti	Salio Benki	Salio la Kwenye Vitabu
1	Miradi ya Maendeleo (60210001176)	471,581,083.54	387,581,083.54
2	Mishahara (60210001174)	38,113,121.32	35,484,302.70
3	Mradi wa Maji (60210004850)	99,748,402.28	96,591,074.93
4	Afya (60210018991)	103,955,005.99	82,823,620.04
5	Elimu (60210018989)	104,668,984.57	76,749,904.57
6	Other Charges (60210001175)	228,367,431.97	164,298,120.03
7	Deposit (60210001177)	362,921,511.05	313,676,788.51
8	Own Source (60210001172)	109,336,945.80	106,636,945.80

b) Akaunti ya Amana

Akaunti ya Amana huweka amana mbalimbali. Wakati tunaanza mwaka huu wa fedha (1/7/2017) mfuko huu ulianza na salio anzia la **Tshs.153,932,076.57** Mapato kwa mwezi Julai - Mei 2018 yalikuwa **Tshs.1,877,385,590.67** na hivyo kuifanya Akaunti hii kuwa na jumla ya **Tshs.2,031,317,667.24** ilipofika tarehe 31/5/2018. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai – Mei 2018 ni Kiasi cha **Tshs.1,717,640,878.73** na hivyo kufanya Akaunti hii kuwa na bakaa ya **Tshs.313,676,788.51**

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

Wakati tunaanza mwaka huu wa Fedha (2017/18), Halmashauri ilikuwa na deni ya **Tshs.570,907,693.76**. Hadi tarehe 31/5/2018 jumla ya deni lenye thamani ya **Tshs.183,570,444.25** lilikuwa limelipwa na hivyo Halmashauri kubakia na deni la **Tshs. 387,337,249.51**

Mh. Mwenyekiti,

Pamoja na Taarifa hii nimefungasha Jedwali Mbalimbali zinazoonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi hiki, Madeni na malipo ya 25% kwa vijiji na kata

Mh. Mwenyekiti,

Naomba Kuwasilisha.

Felisi B. Mhando
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MUFINDI